**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**015/2** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2:30** **Jumatano, 12 Novemba 2014 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

**BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM**

## SEHEMU A: QUR'AN

1. Kwa kutumia tafsiri na mafunzo ya Surat Tyn (95:4-5), fafanua mambo matano yanayoonesha kutukuka na kudunishwa kwa mwanadamu.

2. Eleza vipengele sita vilivyomo katika Qur'an kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu.

3. Andika tafsiri ya Suratu Nasr (idhaajaa) kisha chambua mafunzo matano yatokanayo na sura hiyo.

## SEHEMU B: TAWHIID

4. *Bila shaka Dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. (3:19).* Toa hoja sita kuthibitisha aya hii.

5. *Hakika Mwenyezi Mungu husamehe kushikirishwa; na Husamehe yasiyokuwa haya kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu bila shaka amebuni dhambi kubwa (4:48).*
   Eleza aina kuu nne za shirk kisha onesha kina cha uovu wa shirk kwa mujibu wa Qur'an.

6. Toa hoja sita kufafanua taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku.

## SEHEMU C: FIQH

7. *Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (mwenye kuswali na) mambo machafu na maovu. (29:45)*
   Toa sababu sita zinazowafanya wengi wanaoswali kutofikia lengo hili la swala.

8. Eleza masharti sita anayopaswa kutekeleza muolewaji katika ndoa ya Kiislamu.

9. Wapange wafuatao: maiti, imamu na maamuma katika utaratibu wa swala, kisha onesha hatua kwa hatua jinsi ya kutekeleza swala ya maiti.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D: TAREKH

10. Eleza njia zilizotumika kuwaingiza madarakani Makhalifa wanne waongofu wa Mtume (s.a.w) na mafunzo mawili tunayopata kutokana na njia hizo.

11. "Bila shaka tumekwisha kukupa kushinda kuliko dhahiri" (48:1). Bainisha matukio sita ya kihistoria yanayodhihirisha ushindi wa Dola ya Kiislamu baada ya Mkataba wa Hudaibiya.

12. *Na kwa yakini Tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao Tumekusimulia na wengine Hatukukusimulia (40:78).* Kwa kutumia aya uliyopewa, eleza mambo sita muhimu kwa Waislamu wa leo kujifunza historia ya Uislamu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner